

TATHMINI YA MKAKATI WA MAENDELEO YA KAHAWA 2011- 2021



Utangulizi

- Wadau wa kahawa nchini wanatekeleza mkakati wa miaka kumi wa maendeleo ya zao la kahawa(2011-2021)
- Mkakati huu ulitayarishwa kutokana na azimio la mkutano wa kwanza wa wadau wa kahawa uliofanyika 2009, Mjini Arusha
- Mkakati huu ulitarishwa kwa njia shirikishi ambapo wadau wote katika myororo wa thamani wa kahawa walihusishwa mf. Wakulima, Serikali za mitaa, TCB, vyama vya ushirika, sekta binafsi N.K

Lengo la mkakati huu

- Mkakati huu unalenga kuongeza uzalishaji wa kahawa safi kutoka tani 50,000 hivi sasa, hadi angalau tani 80,000 mwaka 2016 na kufikia tani 100,000 mwaka 2021
- Dhumuni la mkakati huu ni “ *Kuongeza uzalishaji na ubora wa kahawa kitaifa ili kuboresha mapato katika mnyororo wote wa thamani, hususani kwa wazalishaji*”.
- Mkakati wa utekelezaji unaendana na sera za maendeleo za serikali kama vile Mkukuta, ASDP, BRN , Kilimo kwanza N.K

Malengo ya kimsingi ya mkakati

- Kuongeza uzalishaji wa kahawa safi kwa mwaka kutoka wastani wa sasa wa tani **50,000** hadi angalau tani **80,000** kufikia mwaka 2016 na tani **100,000** kufikia mwaka 2021.
- Kuongeza ubora wa kahawa utakaodhihirishwa na ongezeko la bei ya ziada kwenye masoko ya nje kutoka **35%** ya jumla ya uzalishaji ya sasa hadi angalau **70%** kufikia mwaka 2021.
- Hisa ya bei halisi (FOB) ya mkulima kwenye kahawa inayosafirishwa nje iboreshwa kufikia angalau **75%** ifikapo mwaka 2021.

Utekelezaji wa mkakati

Katika lengo kuu la kuongeza uzalishaji utekelezaji ni kama ifutavyo:

MWAKA	ARABIKA	ROBUSTA	JUMLA
2011/2012	21,433	11,625	33,058
2012/2013	35,027	36,180	71,180
2013/2014	27,462	21,306	48,768
2014/2015	25,355	15,865	41,220
2015/2016	35,629	23,816	59,445

Tathmini ya muda wa kati(Mid term review)

- Secretarieti ya mkutano wadau na kamati ya kitaifa ya wadau (NCSC) inapendekeza mkutano huu upitishie azimio kufanya tathmini ya utekelezaji wa mkakati huu
- Tathmini hii inatakiwa kufanyika baada ya kuwa mkakati huu umeshatekelezwa kwa nusu ya muda wa utekelezaji uliopangwa (Miaka 5 kati ya 10)

Tathmini ya muda wa kati (Mid term review)

- Kutambua vikwazo na kupendekeza hatua itakayofuata katika kutekeleza nguzo za mkakati
- Kutambua mabadiliko yanayotakiwa kufanyika kwenye malengo, shabaha na ufadhili na kupendekeza hatua inayofuata

Nawasilisha

Asanteni kwa kunisikiliza